**MTIHANI WA II WA MOKASA 2023**

Hati ya Kuhitimu Kisomo cha Sekondari

**102/3 - KISWAHILI - Karatasi ya 3**

**FASIHI**

**JULAI/AGOSTI 2023 Muda: Saa 2½**

Jina.............................................Nambari ya Usajili...............Darasa.........

Sahihi.....................................................Tarehe...........................................

***Maagizo***

*(a) Andika jina lako na nambari yako ya usajili shuleni kwenye nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
*(b) Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
*(c) Jibu maswali **manne** pekee.*
*(d) Swali la **kwanza** ni la **lazima**.*
*(e) Maswali hayo mengine yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki; yaani Riwaya, Tamthilia, Hadithi Fupi na Fasihi Simulizi.*
*(f) Usijibu maswali **mawili** kutoka **sehemu moja**.*
*(g) Majibu yote ni **lazima** yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*
***(h) Karatasi hii ina kurasa 5 zilizopigwa chapa.***
***(i) Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.***

***Kwa matumizi ya mtahini pekee.***

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | Jumla | |

**1. Lazima**

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

Fahali la dunia ndani ya zizi lake, linatesa
Linaminya
Linanyonya
Kwa kinyama laoneya

Fahali la dunia latumia mabavu, linaoneya
Laandama na kusakama kina mama
Linatesa

Fahali la dunia
Liso na huruma linatesa
Linapiga vindana na wengine wanyama
Tena bila huruma
Laoneya

Fahali hili limeota pembe ziso butu
Limehama zizi, laranda kotekote duniani
Mashariki na kusini, linatesa

Kwa kiburi fahali la dunia linaminya
Linatamba, lajigamba
Lajiona mwamba kwa maguvu
Fahali la dunia lasumbua kwa maonevu
Fahali la dunia lakera wengi insi

Fahali la dunia lidhibitiwe lisitese
Langu malenga sikieni
Dunia unganeni
Pamoja shikaneni, unyonge kataeni
Semeni basi!

Maswali

(a) Thibitisha shairi hili ni la wanamapinduzi. (alama 3)
(b) Eleza dhamira ya mtunzi wa shairi hili. (alama 2)
(c) Utungo huu unakatisha tamaa. Thibitisha kwa mifano mitano. (alama 5)

(d) Huku ukitoa miofano, onyesha jinsi idhini zifuatazo zilivyotumiwa. (alama 3)

i) Inkisari

ii) Mazida

iii) Kuboronga sarufi

(e) Bainisha toni inayotawala kwenye utungo huu. (alama 2)

(f) Nafsi neni katika shairi ni mzindushi. Tetea kauli hii kwa hoja tatu. (alama 3)

(g) Taja tamathali inayojitokeza kwenya kauli 'Semeni basi!' na ueleze umuhimu wake. (alama 2)

**CHOZI LA HERI: JIBU SWALI LA 2 AU 3**

**2.** Sidhani kama moyo wa mja huyu uliwahi kutaka kujua lolote kuhusu ukuaji wangu. Sikumbuki hata siku moja akiniuliza kuhusu neema na mashaka yangu ...

(a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)

(b) Eleza umuhimu wa msemaji. (alama 4)

(c) Eleza namna mrejelewa na wengine wenye majukumu kama yake wanavyofaulu au kutofaulu katika utekelezaji wa majukumu yao. (alama 12)

**3.** Kila alipokuja jijini Jumapili alikuwa kaandamana na wazazi wake kwa ibada.

(a) Eleza nafasi ya mrejelewa katika kuwajenga wahusika wengine riwayani. (alama 8)

b) (i) Bainisha mbinu ya kimtindo katika dondoo. (alama 2)

(ii) Fafanua jinsi mbinu uliyotajwa katika b(i) ilivyotumika kuendeleza maudhui riwayani. (alama 10)

**BEMBEA YA MAISHA: JIBU SWALI LA 4 AU 5**

4. Si neno mama!…Hakuna kizuri kijacho kwa urahisi. Mazuri hutoka mbali na wakati mwingine yana hadithi za kutisha. Maisha yetu ni mfano wa mbegu iliyopandwa. **Mbegu hiyo haina budi kuoza kwanza ndipo ioteshe mche upendezao.**

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (Alama 4)

b) Tambua vipengele viwili vya fani. (Alama 2)

c) Kwa hoja nne, fafanua wasifu wa msemewa. (Alama 4)

d) Ni vipi kauli iliyokolezwa wino inadhihirika katika tamthilia ya Bembea ya Maisha? (Alama 10)

5. (a) " Japo nilipungukiwa na mengi niliyotamani, nilitaka nyinyi muote mbawa mpae juu na kuitazama dunia kutoka kule juu kwa niaba yangu. Stahamala yangu haikunileteа hasara..."

(i) Tambua mandhari ya dondoo hili. (alama 1)

(ii) Bainisha toni inayojitokeza kwenye dondoo. (alama 2)

(iii) Eleza umuhimu wa mandhari ya dondoo hili. (alama 8)

(b) Onyesha jinsi mhusika Sara alivyotumiwa na mwandishi kuendeleza msuko wa tamthilia hii. (alama 10)

**MAPAMBAZUKO YA MACHWEO NA HADITHI NYINGINE: JIBU SWALI LA 6 AU 7**

6. Jadili namna ukiukaji wa haki umeendelezwa katika hadithi zifuatazo. (Alama 20)
   a) Sabina
   b) Kifo cha Suluhu
   c) Nipe Nafasi.

**Pupa: F.M. Kagwa**

7. a) "Pupa imenitumbukiza kwenye kisima nilichochimba, sasa naingia mwenyewe ..."

   i) Bainisha mbinu za kimtindo katika dondoo hili. (alama 2)

   ii) Huku ukitolea mifano mwafaka, onyesha ukweli wa kauli hii. (alama 8)

**Kila Mchezea Wembe: Pauline Kea Kyovi**

   b) "Dunia hii nayo kubwa, anasa zake nyingi huwezi kuzimaliza"

   i) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

   ii) Fafanua toni katika dondoo hili. (alama 2)

   iii) Jadili namna ambavyo anasa imejitokeza katika hadithi hii. (alama 4)

**8. FASIHI SIMULIZI**

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata**

Tumbo: Leo nitakuwa baba na wewe mama. Mimi sipendi mwajificho.

Chausiku: Sawa basi. (Anaimba huku akishika masikio yake) Maskini punda, alinyimwa pembe, akapewa masikio hiyo ndiyo pembe. Pembee pembe, akapewa masikio hiyo ndiyo pembe.

Tumbo: Mamake Chausiku, nahisi njaa. Napeza kula samaki.

Chausiku: Ala! Umejuaje kuwa ninapika samaki? Baba Chausiku, samaki kutoka Soko Mjinga ni tamu kama asali. Chakula ki tayari. (Anampa kitawi chenye vipande vya vijiti). Ndio hii samaki.

Tumbo: (Akiimba) Nimeshiba sana. Asante. Nataka kwenda katika shamba la mahindi kukaza seng'enge. (Anachukua kipande cha mti) Nimechukua nyundo yangu kwenda kujenga ua. (Anatumia kijiti hicho kupigia vijiti vingine ardhini huku akisema kuwa anajenga ua).

Chausiku: Nimechoka sasa. Tuimbe kidogo.

Wote: (Wanaimba huku wakirukaruka)

Watoto wangu ee
Ee
Mimi mama yenu
Ee
Sina nguvu tena
Ee...

**Maswali**

(a) Bainisha utanzu ambapo utungo wa aina hii unapatikana. (alama 1)

(b) Wewe ni mmoja wa wawasilishaji wa utanzu huu wa fasihi simulizi. Eleza sifa unazofaa kuwa nazo. (alama 5)

(c) Eleza sifa zozote **nne** za kipera hiki. (alama 4)

(d) Eleza shughuli **mbili** za kiuchumi zinazodhihirika katika utungo huu. (alama 2)

(e) Unanuia kufanya utafiti kuhusu kipera hiki. Eleza changamoto zinazoweza kukukabili unapotekeleza shughuli hiyo. (alama 6)

(f) Eleza udhaifu wa maandishi kama kifaa cha kuhifadhi data. (alama 2)

*HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA.*

KCSE

Do not write in this margin

THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL,

102/3 FASIHI YA KISWAHILI

Do not write in this margin

Index No .................................. Name: ......................................................................